LEO MAANDIKO HAYA YAMETIMIA

Asante, Ndugu Demos Ndugu Shakarian, au Demos Shakarian na Ndugu Carl Williams, na wajumbe, wote. Nafikiri tu yule ndugu, huyu kijana mlimaji hapa, alinena niliyotaka kunena, usiku wa leo, ya kwamba alichukua usemi wangu moja kwa moja toka kwangu. Kwa sababu, naamini nimeufurahia mkutano huu zaidi ya mkutano wo wote nimewahi kuhudhuria. Sijapata kuona, katika mkutano wo wote, umoja zaidi na ushirika halisi hivyo na upendano wa ndugu. Jambo lingine nimefanya, nimekutana na wajumbe wengi wapya wa Mbinguni, ndugu wapya ambao nimetunukiwa kuamkuana nao kwa mikono na kuwazungumzia.

2 Usiku mchache uliopita, nalikuwa nikimsikiza ndugu huyu Mbatisti. Siwezi kukumbuka jina lake. [Ndugu Shakarian asema, "Irvin."—Mh.] Irvin. Naye akaniletea kadi kutoka . . . naamini ni shangaziye, ambaye anaketi hapa usiku wa leo. Yeye amekuwa na hiyo kadi miaka ishirini.

3 Yeye aliletwa kwenye mkutano, akifa kwa ugonjwa fulani, ambao labda daktari hangeweza kueleza ulikuwa nini. Ni kitu kama ukoma, bali si ukoma. Una . . . Kuna upasuaji, wangekata kitu kama ugwe wa mwili hapa ama cho chote kile, bali angekuwa tu kama mimea, ingempasa kuketi pale. Na alipokuwa ameketi pale, labda kadi yake haikuitwa ama cho chote kile, hakuingia kwenye mstari wa maombi, Roho Mtakatifu akaniongoza kwake. Naye amerudi pale usiku huu, amepata nafuu, nasi tuna shukrani kwa ajili hiyo. Ile . . .

4 [Ndugu Shakarian anasema, "Ndugu, nafikiri—nafikiri Howard Irvin alikuwa pale akizungumza nawe, bali nafikiri shangazi yake yuko hapa. Labda tunaweza kumfanya asimame."—Mh.] Je ungeweza kusimama, sha—shangazi ya . . . ["Ndiye yule. Punga mkono wako. Punga mkono wako." Makutano wanashangilia.]

5 Mungu akubariki dada yangu, kwa ajili ya imani yako hodari katika Mwana wa Mungu. Na Yeye akupe afya hata wakati atakapokuita nyumbani wakati huu wa kufa utakapovaa kutokufa. Ninashukuru sana kwa ajili hiyo, kuwaza ya kwamba alishikilia kadi hiyo kwa miaka hii yote sasa, na ndipo aliletwa hapa kwangu na kuonyeshwa kwangu usiku wa leo. Mnajua, nilikuwa nikisema, na kama mkate juu ya maji, unakurudia, unapojaribu kumtendea mtu fulani kitu fulani.

6 Sasa, nimetunukiwa pia kukutana na wengi wa hawa wahudumu bora na hakika nafurahia ushirika wao mzuri, kushirikiana huku. Ndugu Carl alitangaza mimi nitarudi mwaka ujao, Bwana akipenda, na tukiweko humu duniani. Naam,

natarajia kukutana tena na kila mmoja wenu hapa mwaka ujao na kila mmoja mwanamume kwa mwanamke, alete mjumbe mwingine.

7 Basi kuna jambo fulani ningetaka kusema machache juu yake, labda kwa muda mchache sana.

8 Kwa sababu, Daktari Reed ndiye atakayefuata kuhubiri, nami nimesafiri umbali huo wote kuja humu usiku wa leo, nimesafiri maili mia mbili iii. . .kufanya safari hii, kumsikiza Daktari Reed. Na kitu fulani kilitendeka muda mfupi tu uliopita ambao ninge. . .Lakini—lakini, Daktari Reed, ningesafiri kwa motokaa maili elfu moja kumsikiza yeye. Bali kitu fulani kime. . .Tangu nilipokuwa hapa ningesafiri kwa motokaa maili elfu moja kusikia tu niliyosikia muda mchache uliopita, kitu cha ajabu hivyo, kitu ambacho mwili na damu haviwezi kufunua. Inachukua Roho Mtakatifu kufanya hivyo. Na kuona mtu ambaye aliyafariji maisha yangu hivyo, kwamba hakika ninashukuru maishani mwangu mwote.

9 Niliyotaka kusema, ilikuwa—ilikuwa, kama itanibidi kamwe kufanyiwa upasuaji, na kumwita daktari wa madawa, unaweza kunijia, Daktari Reed, mara moja. Na—naweza kumtumainia kunifanyia upasuaji, ikinibidi kupasuliwa. Mikono inayomwamini Mungu, hiyo—hiyo ndiyo ningetaka inifanyie kazi. Na kwa hivyo sisi. . .natumaini haitanibidi kamwe kupasuliwa. Bali ikiwa nitapasuliwa, ningemtaka yeye, ama mtu kama yeye, kufanya kazi hiyo, iwapo yeye hangekuwako.

10 Kitu fulani kilitendeka kwangu usiku uliopita, ambacho, ama jana alasiri, samahani, ambacho kilikuwa kigeni kwangu. Nami nitanena kwa ufupi, kwa sababu sitaki kuchukua wakati wa ndugu yangu, kwa sababu atahubiri. Bali nakisia ni kama inastahisha ujumbe wangu.

11 Mi-mimi huchunguza mambo madogo. Kila jambo dogo lina maana yake kwangu. Siamini kwamba jambo lo lote linaweza kutukia kwa Mkristo kwa bahati. Naamini limeagizwa na Mungu, kwa sababu Yesu alisema angefanya mambo yote yafanye kazi katika kuwapatia mema wale wampendao Yeye, kwa hivyo basi naamini kwamba kila jambo dogo katika—katika huduma hii dogo na nyenyekevu ambayo Yeye amenipa kuwasaidia ninyi watu, kumsaidia kila mtu, nanyi nyote mmekuwa wasaidizi kwangu, kusaidiana sisi kwa sisi kufikia Utukufu. Kwa hivyo, kila jambo dogo lina maana yake, kwangu mimi. Bali ilikuwa vigumu kwangu kuamini hayo, jana alasiri, nilipopoteza fungu langu la Maandiko hapa juu. Na—nawaambieni, sijapata kamwe kuwa na wasiwasi hivyo maishani mwangu. Na ndipo, bibi ya—yangu alinipa Biblia mpya kama zawadi ya Krismasi.

12 Yangu ya zamani ilikuwa tayari imechakaa. Nimekuwa nayo karibu miaka ishirini sasa, nilipewa na watu wa Houston Gospel Tabernacle, miaka mingi iliyopita, nilipoanza kampeni za injili. Na hivyo basi mimi, naithamini sana, nami . . . vijikaratasi na kurasa, ni kama zavuka, kwa kuvuka bahari, na kwenda huku na huko, hata humu, ni . . . zinapukutika tu. Nami nachukua ukurasa labda katika Mwanzo, na yanibidi kutazama katika Kumbukumbu la Torati mahali fulani kuupata, mwajua, ambapo niliurudisha kwenye Biblia. Kwa hivyo, yeye akanipa moja kama zawadi ya Krismasi. Nami nilichukia kukiweka kando Kitabu cha kale, kimekuwa cha thamani sana kwangu. Nami nikasema, "Kama nikiondoka kabla Yesu hajarudi, kiwekelee juu yangu. Na hebu hiki kizikwe pamoja nami, nami nitafufuka pamoja nacho tutakapofufuka." Kwa hivyo basi, hayo ni maoni yangu, kwa vyo vyote.

13 Kama nilivyozoea kuhadithia hadithi dogo. Natumaini hii si kukufuru. Bali nilienda kwa . . . Mtu fulani aliniambia wakati mmoja, naamini ilikuwa Ndugu Earl Prickett, mkutanoni kule New York; nami nikakutana na mtu fulani akasema, "Aisee, unafanya nini na hawa wafanyi biashara, nawe ni mhubiri?"

Nikasema, "Mimi ni mfanyi biashara."

Naye akasema, "Unafanya biashara gani?"

14 Nikasema, "Assurance" [Dhamana]. Basi akadhani nilisema, "insurance" [bima], mnaona! Kwa hivyo nilisema "Dhamana."

Akasema, "Lo, unauza bima za aina gani?"

15 Nikasema, "Uzima wa milele." Milele! Kasema, "Siuzi. Mimi mwenyewe nina hati ya maagano na ni mwanachama tu, hujaribu kuwaagizia wengine."

16 Nakumbuka kijana mmoja tuliyesoma naye, wakati mmoja, naye alikuwa muuzaji wa bima. Naam, bima ni nzuri, bali mimi sina. Ndipo, basi akaja nyumbani mwangu, na akasema, "Billy, ningetaka kukuuzia bima." Kasema, "Namjua ndugu yako." Ndugu yangu huuza za Metropolitan. Akasema, "Vema," kasema, "Ningetaka, ningetaka kukuuzia bima."

Nikasema, "Naam, Wilmer, asante."

17 Nawe uta . . . huenda yuko hapa usiku wa leo, nduguye, huandika makala kwenye *The Upper Room*, kile kitabu, *The Upper Room*. Basi yeye . . .

Nikasema, "Nina assurance" [dhamana].

Akasema, "Ati nini?"

18 Naye mke wangu akanitazama kama kwamba nilikuwa mnafiki. Yeye . . . nami nikasema . . . kwa hivyo akasema, "Billy?"

Nami nikasema, "Ndio, ee, nina bima."

19 Naye akasema, “Oh, na—na sikitika,” kasema, “Sikujua . . . nilisikia ya kwamba hauna bima yo yote.”

Nami nikasema, “Sivyo, nina dhamana.”

20 Na—naye akanisikia, nilivyosema. Akasema, “Ati umesema nini?”

“Nilisema, ‘Dhamana,’”

Naye akasema, “Vema, unamaanisha nini?”

21 Nikasema, “Ndiyo dhamana, Yesu Bwangu hunipa furaha za mbingu! Mrithi wa wokovu Wake, nimezawa kwa Damu Yake.”

22 Akasema, “Billy, unajua nathamini hilo.” Kasema, “Hilo ni jambo nzuri sana. Bali,” Kasema, “Mwanangu, hiyo haitakutia humu kaburini.”

23 Nikasema, “Bali itanitoa mle.” Siogopi . . . [Ndugu Branham na makutano wanacheka—Mh.] Sijihangaishi jinsi ya kuingia mle; ni kutoka, mnaona. Kwa hivyo nafikiri hivyo ndivyo tunavyojisikia juu ya hayo.

24 Jioni iliyopita, nilipoitwaa ile Biblia, nami singepata lile fungu. Nilitwaa ile Biblia mpya. Nilikuwa nikisoma ile zee. Nami nikatwaa ile mpya na kuiweka kwenye kwapa langu na kukimbia huku. Nami nikafungua mahali hapo, na kuwaza, “Vema, hapa, naamini ilikuwa injili ya Yohana 16:21, na haikusomeka vile kamwe.”

Nikamwambia Ndugu Moore, “Hapo ndipo hayo yalipo?” “Naam.”

25 Nami nikatazama tena, na haikuwa hapo. Ndipo nikawaza, “Naam, wameweka ukurasa mmoja mahali pabaya katika—ukurasa ndani.”

26 Ndipo ndugu yangu hapa akaja, Ndugu Stanley, akaja humu; Askofu Stanley; samahani. Sijui mtu huyu alikusudia nini. Ni—ilinifariji sana haidhuru. Alikuja karibu nami, naye akasema. “Simama imara, ndugu, Mungu huenda labda akafanya jambo fulani.” Waona? Na hiyo ilinifariji vilivyo, kufikiri angesema hayo.

27 Nashangaa iwapo alitambua ya kwamba alitabiri? Bali nilipozungumza naye muda mfupi uliopita, kabla tu sijaja humu, nina hakika alitambua.

28 Basi nikahubiri ujumbe wangu juu ya *Utungu wa Uzazi* na mengineyo. Na njia yangu dogo ya kitoto ya kufanya hivyo, kuhusu yungiyungi; na jinsi linazaliwa mle chini na kukua, nalo linachomoza, na kuvuta jua, na matone ya umande, na mengineyo. Na kisha ndipo uharibifu wa yale linayofia, linayozaliwa kwayo, samahani, linapochomoza. Nami nilikuwa nikitoa mfano wa kanisa.

29 Ni kama tu daktari hapa, kama angaliondoka kwenda kumtibu mgonjwa. Tuna madaktari siku hizi ambao husema,

"Unaweza kusugulia mguu wako, kwenye kisigino, na kuponya kansa iliyo usoni mwako, mnaona." Bali daktari bora hangesikiza mambo kama hayo. Yeye humtibu mgonjwa kulingana na kitabu anachosoma cha utafiti wa madawa.

30 Na hivyo ndiyo ninavyojaribu kufanya kumtibu mgonjwa. Ninapoona kanisa ni ligonjwa, sitaki kujaribu kuwaambia wanahitaji kusalimiana kupya kwa mikono ama cho chote kile, wala dhehebu jipya. Inanipasa kulitibu kulingana na kile Kitabu ambacho nina—ninachojua, mwaona. Na kwa hivyo ninapoona kanisa, likionekana kama limeambukizwa ugonjwa wa surua, nataka wao wanywe Dawa iliyoamriwa ninayojua ni zuri na ni ya surua, kuumaliza kanisani; ninapoona dhambi ikiliambukiza, nitafanya vivyo hivyo!

31 Nilijaribu kulinganisha Esau na Yakobo, ndipo nikaifuatilia hata wakati huu. Na sitaingilia hayo. Bali kuifuatilia hata sehemu ya mwisho kufikia Andiko langu la mwisho nililotumia, nililinganisha, sio kinyume cha Maandiko, bali kama Yesu alivyosema ingekuwa, jinsi yule Daktari mkuu alivyosema hali ya kanisa ingekuwa, katika siku za mwisho, "Ingekuwa ya Ki-laodikia, tajiri, pofu, uchi, kanisa maskini," nayo ingelinganishwa na siku za Sodoma. Sasa, tunajua hiyo ni kweli. Ukichunguza, kihistoria, alitaja siku za Nuhu, kwanza, kisha siku za Sodoma. Na hivyo ndiyo imesafiri, vivyo hivyo.

32 Na historia mara nyingi hujirudia, historia hufanya hivyo, vivyo hivyo pia—vivyo hivyo ahadi za Biblia pia. Kwa mfano, kama katika Mathayo 3, ambapo ilisema, "Kutoka Misri nalimwita mwanangu." Naam, ukifuatilia marejeo kwa hilo, ilikuwa Yakobo, mwanawe, aliyemwita kutoka Misri, huyo alikuwa mwanawe mdogo. Bali mwanawee mkuu. Yesu, aliitwa kutoka Misri, pia. Kwa hivyo ilikuwa na—na maana zaidi ya moja.

33 Kwa hivyo, kisha nilipoona namna walivyoondoka wakinena kuhusu hayo, ndiposa nikaleta mawazo yangu juu ya hilo. Nami nikaondoka kutoka. . .kutoka jukwaani, nikatoka nje. Watoto wangu, tulipokuwa tunaenda nyumbani, walitaka tusimame mahali fulani hapo, kununua sambusa. Nami nikaingia, mke wangu akasema, "Billy, nilipatwa na wasiwasi sana sikujua la kutenda." Kasema, "Mimi ndiye nilikupa ile Biblia."

34 Nikasema, "Si wewe uliyeiandika, na haukuiunganisha kamwe, mpenzi."

35 Yeye akasema, "Lakini, kuwaza tu, ni—nilikupa Bi—Biblia iliyokuwa na kasoro."

Nikasema, "Vema, labda haikuwa nayo."

36 Ndiposa mmoja wa watoto akaichukua, nasi tukaanza kufungua zile kurasa. La, ilionekana nzuri. Bali kule chini kabisa, kurasa mbili zilikuwa zimeshikamana, mnaona, na sura ya 16 ilikuwa upande huu, basi mwendeleo wa sura ya 16 ukaja

upande ule mwingine. Na sura ya 17 ikaanza upande . . . oneni, kamilifu tu, vile vile hasa, kutoka upande mmoja hadi mwingine. Nayo hiyo karatasi ya Kihindi, nyembamba sana, imeshikamana pamoja, nami nilikuwa nikisoma kutoka sura ya 17 wakati wote, badala ya sura ya 16.

37 Nami nikawaza, "Mungu, mbona ukafanya hivyo? Mbona kuwe na jambo kama hilo sasa?" Hayo yalikuwa maoni yangu, mwajua, kuona yote ilikuwa nini, kwa sababu naamini hapana kitu kinachotendeka kwa bahati. Nami nilikuwa nikiwaza juu ya faraja za ndugu huyu hapa akija na kuniambia, "'Uwe imara,' naye ni kasisi, 'uwe imara, huenda ikawa Mungu atatenda jambo fulani," ama jambo kama hilo. Nami nikawaza, "Hiyo ingewezekanaje?"

38 Kisha, nikiketi pale, ikanijia kama radi kutoka Mbinguni. Naam, hii huenda isieleweke kwenu, bali ina maana kwangu, mwaona.

39 Nakumbuka, katika Luka mlango wa 4, kwamba Yesu aliingia sinagogi kule Nazarethi, alikolelewa, na desturi yake ilikuwa kwenda kanisani katika . . . sinagogi, siku ya sabato. Na alipofanya hivyo, tunaona pale ya kwamba kuhani alimpa Biblia, gombo la chuo. Yesu, akitazama kwenye ile gombo, akapata mahali fulani, Isaya 61, naye akasoma hayo Maandiko. Ndipo akamrudishia yule mhudumu ile Biblia. Kisha alipowageukia wale makutano, macho yote yalimwelekea yeye. Naye akasema:

> . . . *Leo Maandiko haya yametimia* . . .

40 Nasi tunajua jinsi somo hilo la Maandiko lilivyokuwa maalum, kwa kuwa alichukua sehemu ya kifungu, cha 1 na cha 2, cha Isaya 61:1 na 2. Bali alisoma kufikia hapa, ambapo, "Roho wa Bwana yu juu yangu, kuwaganga waliovunjika moyo na ku—ku (kuwapa) kuponya wagonjwa, na kuwafungua macho vipofu, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa," kisha akakoma. Kwa kuwa, iliyofuata ilikuwa kuleta hukumu, hiyo ingehusu kuja Kwake mara ya pili, sio kule kuja mara ya kwanza. Na ndipo akakoma, na kugeuka na kusema, "Leo Maandiko haya yametimia." Hiyo ilikuwa wazi jinsi gani!

41 Na ilikuwa—ilikuwa—tamshi jinsi gani kwa waalimu pamoja na wale watu waliokuweko, kwamba Yeye angeeleza hayo wazi wazi kwa watu, "Leo Maandiko haya yametimia." Kwa maana alikuwa hapa, yule Masihi, bali hawakuiamini. Alikuwa hapa, yeye aliyetiwa mafuta kwa ajili ya wakati huo. Kila sehemu ya huduma Yake, kutoka kuzaliwa na kuendelea, Yeye alithibitisha alikuwa nani, na hata hivyo hawangeamini. Ni matamshi jinsi gani! Bali angesema leo . . .

42 Na kama mtu fulani angaliyafungua macho yao, wangalijua, wangalifahamu walikuwa wakiishi siku gani, kwa maana hiyo ilikuwa saa Yake. Kwa maana alikuwa papo hapo akifanya yale

hasa Maandiko, manabii wote, walisema yangetendeka kwenye siku hiyo. Alikuwa hapa ndiye huyo akifanya yale hasa ambayo Mungu alikuwa ametabiri yangetendeka! Je, ni aje basi walikosa kuyaona? Iliwapasa kujua upesi sana wakiona vile huduma Yake ilivyokuwa. Huyo ndiye Masihi. Wangelijua, kwa maana yeye alisema, "Maandiko yametimia."

43 Nawaza juu ya siku hizi. Na tazama hiyo ilikuwa nini kuhani alipotoa Neno. Neno lililosomwa, na likarudishiwa yule kuhani. Na kunukuu kwa mwisho kutoka kwenye soma langu ambalo nilikuwa nalo, na Maandiko yangu niliyoandika, yalikuwa Luka 17:30, ambapo, Yesu akitaja siku hizi tunazoishi, "Wakati wa Laodikia ulio tajiri," na huku umeoza kwa siasa, siasa za kanisa na siasa za taifa, umeoza kupindukia. Na ndipo akasema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa wakati wa mwisho utakapokuja," tazama aliyosema pale, "siku ile atakayofunuliwa Mwana wa Adamu!"

44 Mnaona, "Siku ile atakapofunuliwa Mwana wa Adamu!" Nataka mnisikize kwa makini.

45 Mwaona, Yeye alikuja katika majina matatu. Alikuja kama Mwana wa Adamu, ambaye alikuwa nabii. Na hivyo ndivyo alivyofanya, akathibitisha huduma Yake, kwa kuwa nabii. Sote tunajua hayo. Kila mmoja wetu anajua hayo. Yeye hakusema kamwe alikuwa Mwana wa Mungu, alisema alikuwa Mwana wa Adamu. Sasa siku hizi, Yeye ni Mwana wa Mungu, ambaye alirudi, na sasa yuko katika mfano wa Roho Mtakatifu, Mtu asiyeonekana; bali hata hivyo, Mungu, Mwana wa Mungu. Kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu moja, Yeye ataketi kwenye kiti cha Babaye, ambapo atakuwa Mwana wa Daudi. Yeye alijifunua kwanza kama Mwana wa Adamu, nabii, wakati huu, kupitia kwenye zile nyakati za kanisa, Mwana wa Adamu . . . au Mwana wa Mungu; na katika ule wakati mwingine, Mwana wa Daudi. Wana watatu!

46 Bali unaona hapa, Yeye alisema, katika mwisho wa nyakati za kanisa, ilifikia machafuko sana hata angefunuliwa tena kama Mwana wa Adamu, "atakapofunuliwa Mwana wa Adamu." Kulifaa jinsi gani kule kuchanganyikana jana! Na natumaini hamtaikosa.

47 Tumekuwa na ufunuo wa Mwana wa Mungu, bali ahadi ya mwisho Ibrahimu aliyokuwa nayo kabla mwana hajafanywa . . . ama kuzaliwa, ambaye alikuwa ameahidiwa; kabla yule mwana wa ahadi hajatokea, Mungu alijidhihirisha mwenyewe pale Sodoma kama nabii, akiwa mtu katika mwili, Mungu. Elohim, kama nilivyosikia mtu fulani akilitaja muda mfupi uliopita, ambaye utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani Yake. Yeye alikuwa utimilifu, Elohim ni utimilifu wa Uungu, kwa jinsi ya mwili. Na tunaona pale Lutu alipoona . . . Ibrahimu alipomwona Yeye akija, alisema, "Bwana wangu."

Walikuwa watatu. Na kule chini Sodoma, Lutu aliona wawili, na akasema, "bwana zangu," kutokuwa na ufunuo. Kwa hivyo tazama yaliyotokea hapa, alipokuja, jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe.

48 Je, hatungeweza, je, singeweza kusema haya kama nilikuwa macho, oneni, yule ndugu alitabiri aliponiambia mimi aliyosema! Leo! Tazama aliyofanya mara tu baada ya kusomwa kwa Maandiko hayo, "Siku zile Mwana wa Adamu," si mtu, si binadamu, "Mwana wa Adamu atajifunua mwenyewe miongoni mwa watu Wake tena." Leo ahadi hii, ya majira haya tunamoishi sasa, imetimia machoni mwetu kabisa. Mara Yeye akawageukia makutano, kumi au kumi na wawili, watu wo wote waliokuwa nje kule, haijulikani, Yeye alitenda jambo lile lile alilotenda kule Sodoma. Leo Maandiko haya yamedhihirishwa mbele zenu. Yamefanywa kweli mbele zenu.

49 Basi, ndugu yangu, dada, wajumbe, wahudumu, wo wote walio hapa, watoto wa Mungu, je, tumekaribia vipi kule kuja Kwake basi? Ikiwa sasa tunaona yale Maandiko aliyoahidi, kabla tu moto haujaushukia Sodoma kuuteketeza, na akaulinganisha na siku hii, na tunapoona Andiko hilo likitimizwa mbele ya macho yetu hasa, je, tumekaribia vipi kule kuja Kwake Mwana wa Mungu basi? Je, yale madhihirisho ya Maandiko yamekaribia vipi, kama alivyofanya kwa Ibrahimu, akilileta kanisa kama mfano, ambapo Yeye alikuwa ahadi ya kanisa! Na sasa tunaona, uzao wa Ibrahimu, wa kawaida, jinsi walivyokosea. Bali wazao wa kifalme wa Ibrahimu, ambao ni kwa imani katika Neno lililoahidiwa, sasa wanadhihirishwa duniani siku hizi. Tuko kwenye wakati wa mwisho, ndugu zangu, na dada zangu. Tuko kwenye wakati wa mwisho.

50 Nasi hatuna mfano mwingine. Yanipasa kufananisha Maandiko kwa sababu sina elimu ya kutosha kuleta maneno na kadhalika. Mimi hutoa mifano. Bali kama nimeona katika kivuli . . . Iwapo sijapata kuona mkono wangu kamwe, na nione kivuli chake, ningalijua nilikuwa na vidole vitano. Na hivyo ndivyo inakupasa kuchunguza mifano ya Maandiko ya Agano la kale. Inafanyaje? Inaonyesha haya kimbele. Naye Yesu alisema ya kwamba Sodoma ilikuwa mfano wa wakati wa mwisho sasa. Na Maandiko yale yale yaliyoahidiwa Sodoma, maandiko yale yale yaliyokuwa yakitendeka Sodoma ambayo Yesu alisema yangejirudia leo, yametangazwa papa hapa mbele zetu leo.

51 Mungu awabariki. Msiikose. Na nisipowaona hapa mwaka ujao; wanapokwea vile vipandio vya Dhahabu, natumainia kuwakuta pale juu. Mungu awabariki. [Mahali patupu kwenye ukanda—Mh.]

52 Baba, tuna . . . [Mahali patupu kwenye ukanda—Mh.] Kulingana na Maandiko, tunaona ikidhihirishwa, mbele zetu, ile ishara na mfano wa mwisho. Maneno ya Yesu Kristo yalisema

ndivyo ilivyo. Kama tu ilivyokuwa kule Sodoma, tunaona ulimwengu katika hali yake, tunaona kanisa katika hali yake, tunaona wale—wale wateule wakiitwa kutoka kwenye kila dhehebu; Uhai, ulio mahali hapo, unatoka sasa kutwaa umbo la mbegu. Tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba tutaamka upesi.

53 Kama ndugu fulani alivyosema sasa hivi, aliona mbele ya uso wake, na alipokuwa amefunga macho yake, umati mkubwa ukienda mbele yake. Ee Mungu, tunajisikia ya kwamba kuna umati mkubwa ambao haujaguzwa bado. Tusaidie, Mungu Mpendwa. Na tuondoke katika mkutano huu tukiwa na onyo halisi mioyoni mwetu, tukijua ya kwamba leo Maandiko yametimia. Katika jina la Yesu. Amina.

54 [Ndugu Demos Shakarian anasema, "Halleluya. Mhariri wetu, Jerry Jensen, njoo humu. Mkwewe—mkwewe amepoteza fahamu sasa, na amepata habari hizo sasa hivi. Nao ni wahudumu wa Injili, wahudumu wa Foursquare. Tunaweza . . . Yeye, najua ana huzuni nyingi sana sasa. Na, na tu . . . —Mh.] Amepata hivi sasa, amesikia sasa hivi? ["Naam."] Je wao wako hapa? ["La, wao, wao wako Los Angeles. Wamezirai."]

55 Umbali si kitu kwa Mungu. Yeye ameenea mahali pote. Inampasa kuwa hivyo, kusudi awe Mungu. Baadhi ya mambo makuu sana ambayo najua yanafanyika, katika huduma yangu dogo, ni kwa simu, ama mtu fulani akinipigia simu, mambo makuu sana yametendeka. Hebu tukubaliane pamoja Mungu atawaponya watu hawa ambao ni wagonjwa.

56 Baba yetu mpendwa wa Mbinguni, tunawaleta mbele ya uwepo Wako, kwa maombi. Tunajua ya kwamba usiku mmoja kulikuwako mtume mmoja aliyezuiwa kufanya cho chote wakati huo, alikuwa gerezani na angekatwa kichwa siku iliyofuata. Kule chini nyumbani mwa Yohana Mariko walikuwa na mkutano wa maombi, na mumo humo kwenye hivyo vijumba vya rumade ikaja ile Nguzo ya Moto ambayo iliwafuata wana wa Israeli, ama wana wa Israeli waliifuata jangwani; ikaingia moja kwa moja mle ndani, kwa sababu ya ule mkutano wa maombi na ikafungua kila mlango, na ikamtoa yule mtume nje barabarani tena, akiwa huru kuhudumu.

57 Tunajua kwamba hawa wahudumu, wamishenari, wamefungwa sasa, wamezirai. Bwana, ni Wewe yule jana, leo, na hata milele. Sikia maombi yetu usiku wa leo, Ee Mungu. Ulisema, "Mnapoomba, aminini ya kwamba mmepokea yale mliyoomba, mtapewa." Bwana, tunaamini, na kuomba ya kwamba katika jina la Yesu, ya kwamba wewe utawaponya, Bwana, kwa utukufu Wako imenenwa, imeombwa, naitendwe. Amina.

Bwana awabariki, Ted. Aminini pamoja naye.

58 Ndugu Demos. [Mahali patupu kwenye ukanda, ndipo Ndugu Demo Shakarian anasema, “Je, unamtambua mtu yule?”—Mh.] Hapana, bwana. Amebadilika sana kutoka siku zile, ndugu. [“Njoo hapa, Howard. Alikuwa mtu mwenye sura nzuri sana wakati huo. Yungali mzuri wa uso, Ndugu Branham. Naam, hiyo ni picha nzuri. Nasi tulimsimamisha shangazi wako muda mfupi uliopita pia. Na huenda ikawa ungetaka kusema neno, Howard.” Mahali patupu kwenye kanda]

59 Mtu waliyemsahau; sote tunamfurahia Ndugu Shakarian. Sivyo kila mmoja wetu? [Makutano wanashangilia]

Leo Maandiko Haya Yametimia SWA65-0125
(This Day This Scripture Is Fulfilled)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Lolemba usiku, Januari 25, 1965, katika Inn ya Ramada kule Phoenix, Arizona, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1989 na Urekodishaji wa Sauti ya Mungu.

SWAHILI

©1989 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org